SW

# NomCom

## *Kamati ya Uteuzi*

## Jitolee kwa

# NAFASI ZA UONGOZI WA ICANN

NomCom inakaribisha Taarifa za Nia inapokuwa ikitafuta wagombeaji wa kusaidia katika wadhifa wa kiufundi na kuratibisha sera ya ICANN. Watu wanao nia wanakabirishwa kuwasilisha Taarifa ya Nia kwa kamati ya mwaka huu kwa nafasi zifwatazo:

**HALMASHAURI YA WAKURUGENZI**
KIPINDI CHA MIAKA 3 —— IDADI YA VITI: **2**

**KAMATI KUBWA YA WASHAURI** ALAC
KIPINDI CHA MIAKA 2 —— IDADI YA VITI: **2**
UROPA, AMERIKA KASKAZINI

**MAJINA YA ALAMA YA NCHI INAYOUNGA MKONO BARAZA LA SHIRIK** ccNSO
KIPINDI CHA MIAKA 3 —— IDADI YA VITI: **1**

**MAJINA YA KIKUNDI KINACHOUNGA MKONO BARAZA LA SHIRIKA** GNSO
KIPINDI CHA MIAKA 2 —— IDADI YA VITI: **1**

**Wagombeaji watakaofaulu watachukua nafasi zao mwisho wa Mkutano Mkuu wa Kila mwaka wa ICANN mnamo Novemba 2008.**

Kamati ya ICANN ya Kuteua ni kamati inayojitegemea iliyopewa kazi ya kuchagua wanachama wengi wa Halmashauri ya Wakurugenzi wa ICANN na nafasi zingine katika Mashirika Yanaounga mkono ICANN. ICANN ni shirika la kimataifa, linalofaidi umma, shirika lisilo la kifaida lililojitolea: Kuhifadhi usalama wa kazi na udhabiti wa wavuti, kukuza ushindani; kufikia uwakilishi mpana wa jamii za wavuti duniani; na kusaidia kuanzisha sera kupitia michakato yenye msingi wa maafikiano ya juu-chini. Watu wanaochaguliwa na Kamati ya Uteuzi watakuwa na fursa ya kipekee ya kufanya kazi na wenzi wataalamu kutoka ulimwenguni kote, kushughulikia masuala ya kushangaza ya kuratibisha ufundi wa wavuti na changamoto za kuanzisha sera zenye hali anuwai za utendajikazi, utamaduni na kijeografia, na kupata maoni ya thamani na maarifa kutokana na kufanya kazi katika mipaka ya ufahamu, uwajibikaji na maoni. Wale watakaochaguliwa wataridhika kwa kufanya mchango wa thamana kwa huduma ya umma kuwadia kuendeleza utendajikazi na kubadilisha rasilimali hii muhimu ya dunia. Watasaidia kuhakikisha uthabiti na usalama wa wavuti kwa kazi muhimu sana za jamii.

**KWA HABARI ZAIDI TAFADHALI TEMBELEA TOVUTI YA KAMATI YA UTEUZI:**

## http://nomcom.icann.org

Maombi yatazingatiwa kwa siri. Uteuzi utatangazwa siku 45 kabla ya Mkutano Mkuu wa Kila mwaka wa ICANN mnamo Novemba 2008. Tafadhali tuma maswali au maoni kwa: **nomcom2008@icann.org**

*** Ili Kuzingatiwa Kabisa, Maombi yanapaswa kupokewa kabla ya tarehe 15 APRILI 2008.**

# *Ufafanuzi wa Nafasi za Uongozi Zinazopatikana:*

Wagombeaji watakaofaulu hawalipwi, ijapokuwa gharama za moja kwa moja zilizopatikana wakati wa kazi zitarudishwa. Nafasi hizi zinaweza kujumuisha kusafiri sana kimataifa, pamoja na kuweko binafsi kwa mikutano ya mara kwa mara ya ICANN, na hata pia mawasiliano ya mara kwa mara ya simu na wavuti. Mikutano ya hivi karibuni ya ICANN imekuwa ikifanywa Lisbon, San Juana (PR) na Los Angeles. Mikutano ya 2008 imepangiwa kuwa New Delhi, India, Paris, France, na mkutano wa kila mwaka nchini Afrika (mji TBD). Maeneo haya anuwai huwezesha jamii za wavuti duniani kuhusika. Kamati ya ICANN ya Kuteua imeundwa kufanya kazi kivyake mbali na Halmashauri ya Wakurugenzi wa ICANN, Mashirika Yanayounga mkono, na Kamati za Ushauri. Wanachama wa NomCom hufanya kazi tu kwa niaba ya maslahi ya jamii ya wavuti duniani na kati ya uwezo wa misheni ya ICANN.

## HALMASHAURI YA WAKURUGENZI

Idadi ya Viti: 2
Kuanza kwa Kipindi: Mwisho wa Mkutano wa 2008 wa Kila mwaka
Kuisha kwa Kipindi: Mwisho wa Mkutano wa 2011 wa Kila mwaka

Wakurugenzi wa ICANN, kama kikundi, wanajukumu la kutumia nguvu za ICANN, kudhibiti rasilimali zake, na kutekeleza au kuongoza biashara na mambo yake, isipokuwa kama imetolewa kwenye Vifungu vya ICANN vya Kushirikisha au sheria. Wakurugenzi wanahudumu kama watu ambao wanajukumu la kufanya wanachoamini vyema kuwa kinafaa ICANN na wala sio kama waakilishi wa chombo kilichowateua, waajiri wao, au shirika lingine lolote au mikoa. Wakurugenzi wanatarajiwa kuunga mkono misheni ya ICANN na kufuata Maadili Muhimu ya ICANN.

## KAMATI KUBWA YA USHAURI (ALAC)

Idadi ya Viti: 2 (Uropa, Amerika Kaskazini)
Kuanza kwa Kipindi: Mwisho wa Mkutano wa 2008 wa Kila mwaka
Kuisha kwa Kipindi: Mwisho wa Mkutano wa 2010 wa Kila mwaka

Jukumu la ALAC ni kuzingatia na kutoa ushauri juu ya shughuli za ICANN zinavyolingana na nia za watumiaji wa wavuti. Wanachama wa ALAC wanawezakuwa watu au wanaweza kuwakilisha vyombo ambavyo si vya faida au vya faida, lakini jambo muhimu ni kwamba ni watu. NomCom huchagua wanachama watano wa ALAC, mmoja kutoka kila maeneo matano ya jeografia ya ICANN. Wanachama wa ALAC wanachaguliwa kwa masharti ya mpangilio na nafasi hizi mbili katika mwaka wa 2008 ni za raia wa maeneo ya Uropa na Amerika Kaskazini.

## MAJINA YA ALAMA YA NCHI INAYOUNGA MKONO BARAZA LA SHIRIKA (ccNSO)

Idadi ya Viti: 1
Kuanza kwa Kipindi: Mwisho wa Mkutano wa 2008 wa Kila mwaka
Kuisha kwa Kipindi: Mwisho wa Mkutano wa 2011 wa Kila mwaka

ccNSO ni shirika la kuanzisha sera linalowajibu wa kuanzisha na kupendekeza kwa Halmashauri sera za dunia zinazohusiana na vikoa vya hali ya juu vya nchi (ccTLD), kuanzisha maafikiano kati ya jamii ya ccNSO na kuratibisha na Mashirika mengine yanayounga mkono ICANN, Kamati za Ushauri, na mikoa chini ya ICANN. ccNSO pia uhusika katika shughuli zingine zilizoidhinishwa na wanachama wake, pamoja na kuanzisha shughuli nzuri za kijitolea kwa wasimamizi wa ccTLD, kusaidia katika kukuza ustadi kati ya jamii kubwa ya wasimamizi wa ccTLD, na kukuza ushirikiano wa kikazi na kiufundi kati ya wasimamizi wa ccTLD.

## MAJINA YA VIKUNDI VINAVYOUNGA MKONO BARAZA LA SHIRIKA (GNSO)

Idadi ya Viti: 1
Kuanza kwa Kipindi: Mwisho wa Mkutano wa 2008 wa Kila mwaka
Kuisha kwa Kipindi: Mwisho wa Mkutano wa 2010 wa Kila mwaka

GNSO ni shiraka la kuanzisha sera linalowajibu wa kuanzisha na kupendekeza kwa Halmashauri ya ICANN sera muhimu zinazohusiana na vikoa vya hali ya juu vya vikundi (gTLD). Baraza la GNSO lina mikoa mbalimbali inayowakilisha vikundi fulani vya washikadau na linawajibikaji wa kusimamia uanzishaji sera na michakato ya usimamizi wa GNSO. Mikoa ya GNSO huchagua wengi wa wanachama wa Baraza; NomCom huchagua wanachama watatu wa Baraza kwa masharti ya mpangilio (moja, wakati wa kipindi hiki cha mkutano wa NomCom).

**KWA HABARI ZAIDI TAFADHALI TEMBELEA TOVUTI YA KAMATI YA UTEUZI:**

**http://nomcom.icann.org**

©2008 Internet Corporation for Assigned Names and Numbers tk48763_0108_SW